

Nihusishe !
Hii ni sauti ya mtoto
asiye ona, asiye sikia na
aliye na ulemavu wa
ziada

USHIRIKIANO BAINA YA:

MWEZI WA SITA 2020

Perkins SCHOOL
FOR THE
BLIND



Tanne
Schweizerische Stiftung für Taubblinde
Sinne öffnen, Dialog ermöglichen

Nitazame!

Mimi niko hapa, mimi ni

Mtoto, mwanadamu... kama wewe.

Usiangalie ulemavu wangu, niangalie

Mimi pia, nataka kuwa huru

Labda mimi hutumia muda mrefu kujifunza,

Lakini nina njia yangu maalum

Na kila siku najifunza zaidi na zaidi


Njoo nami tufanye kazi pamoja

Tugundue maajabu yaliyo ndani yangu...



Jambo! Mimi ni mtoto.
Mimi ni sehemu ya jamii,
na jamii kama yangu ziko
kila mahali ulimwenguni.
Mama yangu anasema
kwamba sioni vizuri,
siwezi kusikia vizuri na
nina shida ya kushikilia
vitu... NA:

Mama amepakata mtoto mchanga
ambaye amevaa vifaa vyakumsaidia
kusikia. Wote wanatabasamu.



Nataka kujumuishwa katika shughuli za kifamilia. Kuna njia nyingi ambazo ninaweza kusaidia. Napenda kuwa pamoja na watoto wengine. Napenda maadhimisho ya familia na sherehe za nyumbani. Naweza kusaidia kuchota maji. Naweza kubebwa na babu yangu ndani ya kikapu cha baiskeli yake. Kuna mambo mengi tunaweza kufanya pamoja!

Msichana na mtu mzima wanachota maji pamoja kwenye kisima.


Naweza kushiriki kwenye familia na jamii yangu!

Napenda kucheza na vitu ndani na karibu na nyumba yetu. Tafadhali weka vifaa vya kuchezea mahali ambapo naweza kuvifikia. Nafurahi sana kucheza na watoto wengine. Ninapenda wakati kaka na dada yangu wanapocheza karibu, na mimi hutaka kujiunga nao.

Naweza kucheza!



Mtoto aliyevaa miwani ameketi ndani ya karai na kariby naye kuna kifaa cha kuchezea. Mtoto pia ameshika kifaa cha kucheza cha kutikisa kinacho toa sauti.



Mvulana na msichana wameshikana mikono wakicheza scherzo wa kuruka.

Naweza wasiliana!



Mzazi na mtoto wakiwasiliana kwa kugusa. Mzazi ameketi chini na mtoto amelala chali kati kati ya miguu ya mzazi.. Mzazi na mtoto wanawaliana kupitia kugusa mikono ya mwenzake.

Nataka kuwasiliana nawe.
Ni muhimu sana kwangu -
kama vile kwako.
Wasiliana, cheza na
zungumza nami, kisha
tazama majibu yangu.
Jaribu kujifunza lugha
YANGU, vile najaribu
kujifunza yako. Njoo
tufurahie pamoja!

Naweza kujifunza!

Mtoto na nyanya yake wameketi chini na bakuli ya mboga za majani mbele yao. Kwa pamoja wanachukua majani ya mboga kwenye shina kuandaa chakula.



Ninajifunza kila wakati... ingawa ni kwa hatua ndogo ndogo. Ninaelewa jinsi ya kutumia vitu baada ya kuvipapasa. Ninahitaji mazoezi mengi na wakati mwingi wa kufanya vitu peke yangu. Unaweza kunisaidia kujifunza kwa kuweka utaratibu ambao naweza kufuata kila siku. Na kama watoto wengine, ndio, naweza pia kwenda shule!

Unaweza kunipenda rahisi sana ... na ninakupenda, pia

Kila mtoto anahitaji upendo na utunzaji, mimi pia!
Labda sina jinsi ya kukuonyesha, lakini nakupenda sana. Na ningependa unionyeshe kuwa unanipenda na unanijali. Naweza kuhisi upendo wako.



Kumbuka: Mimi ni mtoto - Zawadi ya thamani

Baba amemshikilia mtoto wake karibu na kubusu uso wa mtoto.



Ndugu na dada wanakumbatiana na kutabasamu.

Nimejaa furaha, uwezo, na machachari na ndoto kama watoto wote. Unaweza kuniona? Mimi niko hapa, katika jamii yetu, katika kitongoji chetu. Mimi ni mtoto anayengoja na anayetaka kupendwa, kuheshimiwa na kujumuishwa. Kama unanithamini na kunitia moyo, wengine kwenye jamii watafanya vivyo hivyo! Wakati mmoja kulikuwa na mtoto kama mimi. Alikua ni mwanamke mashuhuri anayeitwa Helen Keller, na akasema "peke yetu tunaweza kufanya kidogo; kwa pamoja tunaweza kufanya mengi." Nina ndoto nyingi- utanisaidia kuzitimiza?